**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI (R) (MST.) SEMISTOCLES S. KAIJAGE KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO CHA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI NA VYAMA VYA SIASA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA MWL. J. K. NYERERE**

**TAREHE 19 AGOSTI, 2020**

- **Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume,**
- **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Sera, Bunge na Uratibu),**
- **Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Siasa,**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**
- **Mkurugenzi wa Uchaguzi,**
- **Mwakilishi kutoka Jeshi la Polisi**
- **Mwakilishi kutoka Uhamiaji**
- **Mwakilishi kutoka TAKUKURU**
- **Watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Wanahabari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

*Tumsifu Yesu Kristo, Asalam Aleikum*

Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwakaribisheni wote katika kikao hiki muhimu, ambacho ni sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020. Viongozi wa vyama vya siasa mnakumbuka tulikutana hapa tarehe 1 Agosti, 2020 kwa ajili ya kupeana taarifa ya maandalizi ya uchaguzi katika maeneo mbalimbali ikiwemo, taarifa ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura, taarifa ya idadi ya majimbo, maadili ya uchaguzi na kampeni, ununuzi wa vifaa, bajeti ya uchaguzi mkuu, elimu ya mpiga kura na mialiko ya watazamaji wa uchaguzi.

Kama nilivyotangulia kusema, kikao chetu cha leo kina tukutanisha na wadau wengine muhimu katika utekelezaji wa michakato mbalimbali ya uchaguzi kama vile Jeshi la

Polisi, Jeshi la Uhamiaji, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa( TAKUKURU) Msajili wa vyama vya siasa, Taasisi ya Mwalimu Nyerere na Viongozi wa dini.

Hatua hii imefikiwa kutokana na maombi yenu ya kupata wasaa wa kukutana na wadau wengine muhimu wa uchaguzi hasa katika kipindi kama hiki. Lengo la kukutana huku, nikupata nafasi ya kufahamu wajibu wa wadau wengine wakati wa uchaguzi, lakini pia kujadiliana namna bora yakufanikisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, na hatimaye kuweza kuwa na uchaguzi huru, wa haki, wa kuaminika na utakaofanyika katika mazingira yenye usalama na amani.

**Ndugu viongozi wa Vyama vya Siasa**

Katika kikao cha leo tutapata mada kutoka Jeshi la polisi ambao ni wadau muhimu katika kuhakikisha uchaguzi unafanyika katika mazingira salama yanayodumisha amani katika kipindic hote cha mchakato wa uchaguzi.

Masuala ya uraia vile vile yamekuwa ni changamoto katika chaguzi hasa katika maeneo ya mipakani ambako mwingiliano wa watu kutoka nchi jirani ya Tanzania umekuwa ni mkubwa.  Kutokana na mazingira haya, Tume imeona ni vyema ikamwalika mdau mwingine muhimu ambaye ni kutoka Jeshi la Uhamiaji ili awe kuzungumza nanyi kuhusu masuala ya uraia na changamoto zake hususan katika kipindi hiki tunapoelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Katika kikao chetu pia tutasikia kutoka TAKUKURU. Kama tunavyofahamu rushwa ni adui wahaki, kwani pamoja na mapambano yanayoendelea bado kuna malalamiko ya kuwapo kwa vitendo vya rushwa katika chaguzi, hivyo ni matarajio ya Tume kwamba uwepo wao hapa utatoa nafasi ya kujadili namna bora ya kupambana na kuzuia rushwa katika chaguzi.

Eneo lingine ambalo mtapata nafasi ya kusikiliza ni kuhusu gharama za uchaguzi na utaratibu wake.  Mwakilishi kutoka ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa atazungumza nanyi juu ya utekelezaji wa Sheria ya Gharama za uchaguzi.

Taasisi ya Mwalimu Nyerere pia imealikwa katika kikao hiki ili, pamona na mambo mengine wazungumze masuala mazima yanayohusu na kugusa Amani katika Uchaguzi.  Kama tunavyofahamu bila ya kuwapo kwa mazingira tulivu na ya Amani uchaguzi hauwezi kufanyika na ushiriki wa wananchi unakuwa wa mashaka.

Vivyo hivyo katika kikao hiki tuna viongozi wa dini.  Kama tunavyofahamu viongozi wa dini wana nguvu kubwa ya ushawishi katika jamii na wana namna bora ya kuwafikishia ujumbe waumini ama waamini wao. Kwa hiyo, leo na wao wanayofursa

ya kutueleza nafasi ya viongozi wa dini katika kufanikisha uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

**Ndugu viongozi wa Vyama vya Siasa**

Pengine nitumie nafasi hii pia, kuwataarifu kuwa zoezi la uchukuaji fomu limeendela vizuri. Hadi sasa jumla ya vyama vya siasa 17 tayari vimechukua fomu za uteuzi kwa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hivi sasa vyama na wagombea wao, wanaendelea na zoezi la kutafuta wadhamini mikoani, ili kutimiza sehemu ya masharti ya uteuzi. Tume inavipongeza vyama vyote vya siasa vilivyosimamisha wagombea, kwa kuonesha nia ya kutimiza haki yao ya msingi ya kikatiba ya kuchaguliwa. Kitendo hicho ni kielelezo muhimu cha kukuza na kutekeleza demokrasia nchini.

Kwa upande wa uchaguzi wa wa bunge na madiwani uchukuaji wa fomu ilioanza tangu tarehe 12 Agosti, 2020 unaendelea. Zoezi hili litaendela hadi tarehe 25 Agosti, 2020 ambayo itakuwa ni siku ya uteuzi kwa wagombea wa ngazi zote.

**Ndugu viongozi wa Vyama vya Siasa**

Kwa kumalizia, nirudie kuwashukuru viongozi wa vyama vya siasa, kwa kukubali mwaliko licha ya shughuli nyingi za kichama mlizonazo wakati huu,na kwaniaba ya Tume niwatakie kila la kheri katika hatua zinaofuata, ikiwemo urejeshaji wa fomu za uteuzi.

Tume pia inatoa shukrani kwa watakao wasilisha mada leo kutoka viongozi wa Dini, wawakilishi kutoka TAKUKURU, Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Msajili wa Vyama Vya Siasa kwani mafanikio ya uchaguzi wowote unaanza na wadau kuwa na ulewa wa pamoja na lengo moja la kuhakikisha nchi yetu mwaka 2020 inakuwa na uchaguzi huru, wa haki, amani na wa kuaminika kwa mustakabali wa demokrasia ya nchi yetu.

***Baada ya kusema maneno hayo machache, sasa natamka kuwa kikao chetu kimefunguliwa rasmi***

**Asanteni kwa kunisikiliza**